JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/308
Fax Na: 2152820
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Kamishna wa Mamlaka )*

Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 80327,
**DAR ES SALAAM.**

# TAARIFA KWA UMMA

## WATU WAWILI WAKAMATWA WAKISAFIRISHA DAWA ZA KULEVYA AINA YA HEROIN

**Dar es Salaam, 04 Februari 2020:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya. Watu hao ni **STANLEY SALVATORY NGOWI** ama **SULTAN SALVATORY NGOWI** mwenye umri miaka 24 kabila **Mchaga** mkazi wa Tabata Segerea na **JIMMY WALTER MLAKI** mwenye umri wa miaka 24 kabila **Mchaga** mkazi wa Kinondoni Dar es Salaam.

Watuhumiwa walikamatwa maeneo ya **Kibo Ubungo** tarehe **27/01/2020** wakiwa na gari aina ya **SIENTA** rangi ya **Silva** yenye namba za usajili **T776 DSE.** Maafisa wa Mamlaka walifanya upekuzi kwenye gari hilo na kukamata unga ambao baada ya uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ulithibitika kuwa ni dawa za kulevya aina ya **Heroin** wenye uzito wa **gramu 508.163**. Pia maafisa wa Mamlaka walikamata mzani (digital scale) pamoja na nyaraka mbalimbali. Watuhumiwa wanatarajiwa kupelekwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa.

Ukamataji huu umefanyika kutokana na mtego uliowekwa na Mamlaka maeneo ya **Kibo Ubungo** baada ya kupata taarifa ya uwepo wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya

eneo hilo. Katika harakati za ukamataji watuhumiwa wengine wawili walitoroka na Mamlaka inaendelea kuwafuatilia.

**Mamlaka** inawakumbusha watanzania wote hususan vijana ambao ndio kundi kubwa linalodanganyika na kujihusisha na dawa za kulevya kuwa, kujihusisha kwa namna yoyote ile na dawa za kulevya ni kosa kisheria. **Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya [Sura ya 95]** inatoa adhabu kali hadi kifungo cha maisha kwa atakayebainika kujihusisha na biashara hiyo. Hivyo, **Mamlaka** inaendelea kuwasihi Watanzania kutojihusisha kabisa na biashara hii haramu wala matumizi ya dawa za kulevya kwani atakayeshiriki atachukuliwa hatua stahiki za kisheria.

Imetolewa na,

Lilian B. Matho,
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**,**
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**